

chenu kimekaidi kutekeleza matakwa ya kifungu cha 9(2)(e) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, hivyo kimepoteza sifa za usajili na kukiuka Sheria ya Vyama vya Siasa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inatumia fursa hii kukufahamisha wewe na wanachama wengine wote wa Democratic Party, nia ya Msajili wa Vyama vya Siasa kufuta usajili wa kudumu ^{wa chama} chenu Democratic Party, kutokana na kupoteza sifa za usajili na kukiuka Sheria ya Vyama vya Siasa.

Kifungu cha 19(1)(2)(a) na (b) kinasema ifuatavyo, nanukuu:-

"19-(1) Subject to subsection (2) the Registrar may cancel the registration of any political party which has contravened any of the provisions of this Act or which has otherwise ceased to qualify for registration under this Act.

- (2) The Registrar shall not cancel the registration of any party unless—*
- a) he has, in writing, informed the party concerned of the contravention or the loss of qualification and of the intention to cancel the registration;*
 - b) he has received or failed to receive, within the period prescribed by him, any representations from the party concerned."*

Hivyo, Msajili amewapa siku kumi na nne (14) tu, kuanzia tarehe ya barua hii, kuwasilisha maelezo, kwa nini usajili wa kudumu wa chama chenu usifutwe, kwa kukosa sifa za usajili na kukiuka Sheria ya Vyama vya Siasa, ilivyoelezwa hapo juu.

Wako katika ujenzi wa Taifa.



Sisty L. Nyahoza

Kny: **MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**